TANGAZO LA SERIKALI Na. 503 la tarehe 21/6/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAZIWA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Maziwa ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto;

"maziwa" maana yake ni-

(a) inapotumika kuhusiana na mfugaji, mfugaji yeyote ambaye anajihusisha na shughuli ya kuuza maziwa kama atakavyoyatoa nyumbani kuyapeleka vituo vya kukusanyia maziwa;

(b) inapotumika kuhusiana na mnunuzi, mtu yeyote anayejihusisha na shughuli ya kununua maziwa kama atakavyoyanunua kutoka kwa mfugaji au mtu yeyote kutoka katika eneo la Halmashauri;

(c) inapotumika kuhusiana na mmiliki wa vituo vya kukusanyia maziwa ina maana ya mmiliki huyo kutumia maziwa hayo kama malighafi katika kiwanda cha mmiliki husika; na

(d) inapotumika kuhusiana na taasisi ya umma au serikali au ya mtu binafsi au kampuni, maana yake ni taasisi au kampuni hiyo inayojihusisha na biashara ya maziwa;

"mfugaji" maana yake ni mtu yeyote ambaye anajishughulisha na shughuli za ufugaji katika eneo la Halmashauri na ambaye anauza maziwa katika vituo vya kupokelea maziwa;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza kazi za Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

"mnunuzi" maana yake ni mtu yeyote anayenunua maziwa na inajumuisha ushirika, kampuni, taasisi au mtu binafsi anayenunua maziwa ghafi kwa ajili ya usindikaji;

"ushuru" maana yake ni ushuru wa maziwa utakaotozwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Wajibu wa Halmashauri

**4**.-(1) Halmashauri itatoza kwa mnunuzi ushuru wa maziwa kwa kiwango cha asilimia tatu ya bei ya kununulia maziwa katika vituo vya kukusanyia maziwa.

(2) Ushuru utalipwa kwa Halmashauri au wakala aliyeteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri.

Kibali

**5**.-(1) Mnunuzi wa maziwa atapaswa kuomba kwa Halmashauri kibali cha kusafirisha maziwa.

(2) Kila mnunuzi wa maziwa atawajibika kuingia mkataba maalumu na Halmashauri wenye masharti na taratibu za ununuzi wa maziwa.

(3) Endapo Halmashuri itaona inafaa, itakipa kijiji mamlaka ya kutoa vibali vya ununuzi wa maziwa ili kurahisisha zoezi la ukusanyaji wa maziwa.

(4) Kibali cha kusafirisha maziwa kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Uteuzi wa Wakala

**6**.-(1) Halmashauri inaweza kuteua wakala kwa ajili ya kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Rejesta ya mnunuzi wa Maziwa

**7**.-(1) Kutakuwa na rejesta ya mnunuzi wa maziwa katika kila kituo cha kukusanyia maziwa.

(2) Kila kituo au kijiji cha kukusanyia maziwa kitatunza rejesta kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za wanunuzi wa maziwa.

Wajibu wa mfugaji

**8**. Mfugaji ambaye chini ya Sheria Ndogo hii ni muuzaji wa maziwa, atakuwa na wajibu wa kupeleka maziwa katika kituo cha kukusanyia maziwa.

Kutolipa ushuru wa maziwa

**9**.-(1) Endapo mnunuzi atashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, maziwa yatakamatwa na kuhifadhiwa kwa saa kumi na mbili na baada ya muda huo kupita bila ya mnunuzi kuyakomboa maziwa hayo yatauzwa kwa njia ya

mnada.

(2) Masharti katika kanuni ndogo ya (1) yatatekelezwa baada ya Halmashauri kupata idhini ya mahakama.

(3) Halmashauri itachukua ushuru katika fedha zitakazopatikana kutokana na mauzo ya maziwa yaliyokamatwa na kunadiwa chini ya kanuni ndogo ya (1), gharama za utunzaji wa maziwa kwa wakati wote maziwa yalipokuwa chini ya uangalizi wa Halmashauri pamoja na gharama za mnada, na kiasi kitakachobaki kitarudishwa kwa mnunuzi.

Maziwa kupoteza thamani

**10.** Endapo maziwa yaliyokamatwa chini ya kanuni ya 9(1) yatapoteza thamani, Halmashauri haitahusika na upotevu wa thamani katika maziwa hayo yaliyo chini ya uangalizi wake, isipokuwa kama kupoteza thamani kumesababishwa na Halmashauri au wakala.

Makosa

**11**. Mtu anatenda kosa ikiwa-

(a) anashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) anamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ushuru;
(c) anashindwa kuhifadhi kumbukumbu ikiwa ni pamoja na rejesta ya maziwa na hesabu zinazohitajika chini ya Sheria Ndogo hii; au
(d) anamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

.

Adhabu

**12**. Mtu atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

**13**. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ushuru anaodaiwa

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(4))*

KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZIWA

Jina la mwombaji ………….…..…………….…………………..…
Anwani ya mwombaji ………..…………………………………….
Tarehe ya maombi …………..…………………………………..…..

Kibali kinatolewa kwa ajili ya kufanya shughuli kama ulivyoomba kwa mujibu wa Sheria. Kibali hiki ni kwa ajili ya kusafirisha maziwa nje ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

MAELEZO YA MAZIWA YANAYOSAFIRISHWA NJE YA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO
Jina la mwenye gari …………………………………………..…………….
Jina la Dereva …………………………………………………………...………
Saini ya Dereva ………………………………………………………………
Kiasi cha Maziwa yanayosafirishwa (tani/lita) ……………………………………
Sehemu/kampuni/mfugaji/ushirika/mmiliki wa maziwa ……………...………
Hali ya Maziwa (hayajachakatwa, yamechakatwa, nyingine taja) …………..………
Yanakopelekwa/kusanywa ………………………………………………………
Jina la Mnunuzi ……………………………………………………………..…
Aina ya usafiri (taja pamoja na namba za usajili) ……………………………..…

MAONI YA AFISA MWIDHINIWA
Kibali kimetolewa kwa ……………………………………
Ushuru wa maziwa umelipwa/ haujalipwa …………………………………………
Stakabadhi namba .……………………………………………………………
Jina la Afisa Mwidhiniwa …….……………………………………………………
Cheo/Wadhifa ………………………………………..………………………
Tarehe ……………………………………………………………………………..

(N.B) kibali kijazwe nakala mbili. Nakala moja kwa ajili ya msafirishaji na nyingine iwasilishwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W).

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 13)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Maziwa za Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ya Mwaka, 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, Niko tayari kulipa kiasi cha ushuru na faini ninayodaiwa badala ya kupelekwa mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….………….

Jina……………………………….. Saini…………………………………….

MBELE YANGU :
Jina: …………………………………..……………………
Saini……………………….………………………..………
Wadhifa: ………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imebandikwa katika hizi Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kufuatia Azimio la kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kilichofanyika tarehe 12/5/2023 na kushuhudiwa,

Lakiri imebandikwa mbele ya:-

IKUPA H. MWASYOGE,
*Mkurungenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Lushoto*

MATHEW MBARUKU,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Lushoto*

**NAKUBALI**,

**L.S**

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*,